January 24, 2024

Mch. Almodad Amos

# 02. Ushindi Katikati ya Kushindwa

Moja kati ya mambo ya muhimu sana utakayojifunza kupitia Kitabu cha Danieli na Ufunuo ni kwamba: Mungu wetu huwa hakutwi na majanga kwa kushtukizwa. Huwa anayaona kutokea mbali na daima huwa anakua ameshaweka mpango maalum wa kuwasaidia na kuwaokoa watu wake.

Tutaliona hilo katika somo letu la leo tutakapokua tukijifunza Somo hili ambalo linatupatia utangulizi na msingi, wa Kukielewa kitabu cha Danieli, na kumtambulisha kwetu mwandishi wa Kitabu hicho.

## Watu Maarufu Waliosoma Unabii wa Danieli

Kama unadhani Kitabu cha Danieli ni kwa ajili ya watu waliokosa kazi, ni vyema utafakari upya kwa sababu hiki Kitabu kwa sababu ya umuhimu wake, kimewavuta wengi kukisoma na kukichunguza:

- Albert Einstein: Huyu alikua mwana-fizikia mbobezi ambaye wataaluma wa fizikia wanamuita Baba wa Fizikia ya Kisasa. Hakua Mkristo lakini alikisoma Kitabu cha Danieli na akaamini kinajibu maswali yake mengi ya kisayansi yaliyomsumbua.
- Isaac Newton: Huyu alikua mtaalam wa Hesabu na Fizikia. Aliandika Fafanuzi (Commentary) ya Kitabu cha Danieli.
- Napoleon Bonaparte: Huyu alikua Mfalme na Kamanda wa majeshi ya Ufaransa katika Karne ya 19, aliamini katika unabii wa Kitabu cha Danieli.
- Martin Luther: Mwandishi wa vitabu, mwana-teolojia, mtunzi wa nyimbo na profesa wa Chuo Kikuu; alipenda kusoma na kujifunza kitabu cha Danieli.

Kwa hiyo kama umeanza safari ya kujifunza Kitabu hili, hauko peke yako. Uko katika msitari wa maelfu ya watu ambao wanautafuta uso wa Mungu na kutamani kujua kile alichokipanga kwa ajili yetu, hasa katika zama hizi za wakati wa mwisho.

## Utambulisho wa Danieli

Kwa hiyo sasa Danieli alikua nani? Kwa mujibu wa maneno ya Yesu katika Mathayo 24:44, Danieli, alikua nabii.

- Danieli ni Jina la Kiebrania linalomaanisha, "Mungu ni Hakimu/Mwamuzi Wangu."
- Jina jingine anaitwa Belteshaza
- Nyumani kwake ni Yudea, lakini sehemu kubwa ya Maisha yake yalitumika huko Babeli.
- Hakuna mengi yanayosimuliwa kuhusu familia yake, isipokuwa kwamba alizaliwa katika Ukoo wa Kifalme katika kabila la Yuda.
- Danieli alikua Kiongozi mkubwa wa Serikali, Waziri Mkuu wa falme mbili (Ufalme wa Babeli na Uajemi) na wakati huo huo alikua Nabii.
- Huyu ndiye mwandishi ambaye aliandika Kitabu cha Biblia kinachoitwa Kitabu cha Danieli.
- Kwa kipindi flani, wakati Danieli alipokua nabii, Yeremia na Ezekieli pia walikua manabii katika wakati huo huo. Danieli alifanya kazi yake kama nabii kuanzia mwaka 605 - 536 K.K.
- Danieli alikua mtu mwenye Ujasiri mwingi katika Imani, Maombi endelevu na msimamo wa kiroho usioyumba wala kutikisika, hata wakati alipotishiwa kifo. Danieli ni mfano mzuri wa kile ambacho Mungu anaweza kuwatendea watoto wake waaminifu.
- Moja kati ya mambo yanayoshangaza sana kuhusu Danieli, ni namna alivyokua Waziri Mkuu, katika mataifa mawili ya siyopatana na wakati huo huo akiwa mtumwa katika nchi ya ugenini.

Sasa nini kilitokea mpaka Danieli atoke kuwa Mtoto wa Kifalme, awe mtumwa na Kisha awe Waziri Mkuu. Ni kisa kirefu lakini ktk utangulizi huu ngoja nikudokeze mambo mahache.

## Danieli Apelekwa Utumwani

Kitabu cha 2 M. Nyakati 35:20–24 kinaonyesha moja ya wafalme wazuri kabisa wa Israeli aliyeitwa Yosia, alitoka kwenda kupigana vita na Farao katika Bonde la Kakemishi, na katika vita ile Yosia alikufa. Wakati watu wanamuombolezea Yosia, Nabii Yeremia anapokea unabii kutoka kwa Mungu unaowakataza watu kumlilia Yosia na badala yake kujililia wao wenyewe, maana msiba uliokua unakuja mbele yao ulikua mkubwa zaidi. Walikua wanakwenda kupelekwa utumwani kwa sababu ukaidi wao kwa neno la Mungu.

Baada ya Farao kumuua Yosia, Farao naye aliendelea katika vita dhidi ya majeshi ya Nebkadneza wa Babeli, na safari hii Farao alipigwa na kushindwa vibaya. Baada ya kumshinda Farao Nebkadreza aliamua kupita Yuda na kuipiga pia, lakini wakati vita hii inaendelea, Nebkadreza alipokea habari kwamba Baba yake Nabopolasa alikua amekufa na hivyo akawahi kwenda nyumbani ili kulinda na kurithi kiti cha ufalme. Wakati anaondoka aliacha maagizo kwa viongozi wa jeshi kwamba waipige Yuda na wateke mateka, na hapo ndipo tunapokuja katika Kitabu cha Danieli 1:1 - 4.

> Danieli 1:1 - 4 Katika mwaka wa tatu wa kumiliki kwake Yehoyakimu, mfalme wa Yuda, Nebukadreza, **mfalme wa Babeli**, alikwenda Yerusalemu akauhusuru. 2 **Bwana akamtia Yehoyakimu**, **mfalme wa Yuda, katika mkono wake**, pamoja na baadhi ya vyombo vya **nyumba ya Mungu**; naye akavichukua mpaka nchi ya Shinari, mpaka **nyumba ya mungu** wake; akaviingiza vile vyombo katika nyumba ya hazina ya mungu wake. 3 Mfalme akamwambia Ashpenazi, mkuu wa matowashi wake, awalete baadhi ya wana wa Israeli, **wa uzao wa kifalme**, na wa uzao wa kiungwana; 4 vijana wasio na mawaa, wazuri wa uso, wajuzi wa hekima, werevu kwa sababu ya maarifa yao, wenye kufahamu elimu, watakaoweza kusimama katika jumba la mfalme; tena alimwambia awafundishe elimu ya Wakaldayo, na lugha yao.

## Dhima Kuu ya Kitabu cha Danieli

Aya za kwanza kabisa katika Kitabu cha Danieli, zinatupatia nuru juu ya kile kinachozungumziwa katika Kitabu kizima. Zingatia mambo yafuatayo:

1. Kuna pande mbili hapa ambazo zinapingana. Kuna Mungu wa mbinguni, na kuna mungu wa herufi ndogo; Kuna miji miwili hapa, Yerusalemu (ambayo ndio makao makuu ya Yuda) na kuna Babeli, na hatimaye kuna Mfalme wa Yerusalemu na Mfalme wa Babeli.
    - Katika kujifunza unabii, Babeli inawakilishi machafuko, uasi, na upagani. Wakati Yerusalem ikiwakilisha mahali ambapo Mungu anatawala.
    - Inavyoonekana hapa ni kama Babeli inapata ushindi, na ni kama watu wa Mungu wanaonekana kushindwa.
    - Inaonekana kama mungu wa kipagani anapata ushindi, dhidi ya Mungu wa Mbinguni.
    - Moja kati ya maswali makubwa ambayo yatajibiwa na Kitabu cha Danieli, ni kwa nini uovu unaonekana kama vile kwa sasa umepata nguvu na unashinda? Kwa nini watu wasiopokea maadili mema ndio wanaonekana kupata ushindi wakati watu wa Mungu mambo yao yanaonekana kwenda mrama?
2. Lakini kama utachunguza vizuri hapa ushindi ambao Nebkadreza anaupata hapa, unakuja kwa sababu Biblia inasema Bwana alimtia Yehoyakimu katika Mkono wa Nebkadreza. Na kwa hiyo tunaweza kusema, mambo hayakua yanatokea kwa bahati mbaya, hata katikati ya majanga na shida bado huwa kuna mkono wa Mungu ambao unaongoza, unapima, unaruhusu na unatawala mambo yanayowapata na kuwatokea wanadamu hapa duniani. Moja kati ya mambo makubwa kabisa tunayojifunza katika Kitabu cha Danieli ni kwamba Mungu wetu hajawahi kuiacha dunia iende vyovyote utakavyoenda, bado ameketi katika kiti chake cha enzi, na bado anatawala.

Kitabu cha Danieli kinaanza kwa huzuni lakini kinaisha kwa ushindi mkubwa. Danieli 12:1 - 3 inaonyesha kwamba wakati wa Mwisho Mungu atawaokoa watu wake na kuwapatia thawabu milele na milele.

## Picha Pana ya Kitabu cha Danieli

Muhtasari mzima wa Kitabu cha Danieli unawekwa katika Danieli 1:1 - 4, na Danieli 12:1 - 3. Sura za kwanza zinaonyesha namna ambavyo Mfalme wa Kipagani ataonekana kupata nguvu dhidi ya watu wa Mungu, lakini Sura ya kumi na mbili inaonyesha namna ambavyo mwisho wa mambo yote kutakua na ushindi kwa watu wa Mungu.

Sura zilizopo katikati ya Kitabu cha Danieli zinaonyesha uzoefu ambao Mungu ataruhusu watu wake waupitie katikati ya pambano lililopo kati ya Ufalme wa Mungu na ufalme wa Shetani.

Kwa kipindi kifupi, itaonekana kama Shetani anapata nguvu, lakini ni kwa sababu Mungu amemruhusu afanye yale anayoyafanya ili ulimwengu mzima ushuhudie ubaya na madhara ya kuichagua dhambi na kumkataa Mungu.

Wakati huo huo, ambao Shetani ameachwa adhihirishe makucha yake, Kitabu cha Danieli kinatuonyesha namna Mungu anavyowaongoza na kuwasaidia watu wake kushughulika na majaribu, vitisho na mateso ambayo Shetani atayatumia ili kuwafanya watu wa Mungu kuitupa imani yao.

Kumbuka ahadi ya Mungu:

> Amos 3:7  Hakika Bwana MUNGU hatafanya neno lo lote, bila kuwafunulia watumishi wake manabii siri yake.

## Danieli Aitwa Kuwa Nabii wa Mungu

Danieli anakadiriwa alikua na miaka 15 wakati alipochukuliwa, yeye na wenzake, kwenda utumwani Babeli. Hakuwa amejua matukio gani hasa yangetokea mbeleni, lakini aliendelea kumwamini Mungu, na hatuoni neno lolote la kumlaumu Mungu likitoka kinywani mwake.

Ilionekana kama amepoteza ndugu zake, Ibada alizozizoea zilionekana kuondolewa kwake. Inaonekana kama alipoteza kila kitu. Lakini pamoja na hayo naomba ujifunze yafuatayo kwa Danieli:

### 01: Hata Ukipoteza Kila Kitu cha Dunia Hii Usikubali Kuipoteza Imani yako.

> Daniel 1:8  Lakini Danieli aliazimu moyoni mwake ya kuwa hatajitia unajisi kwa chakula cha mfalme, wala kwa divai aliyokunywa; basi akamwomba yule mkuu wa matowashi ampe ruhusa asijitie unajisi. .

Danieli alikua amepitia majaribu makali katika umri mdogo kabisa. Alitengwa na jamii yake, alitengwa na utaratibu wa ibada alizozizoea, alitengwa na utamaduni aliouzoea, aliona ndoto zake za maisha zikipotea, alitengwa na fahari ya uzao wa kifalme na akawa mtumwa; lakini bado katika hali zote hizo inaonekana moyoni mwake aliazimia kuendelea kuishi kulingana na maelekezo ya neno la Mungu, hata akiwa katika huzuni na wakati mgumu.

Fundisho kwetu ni kwamba, hali ngumu na maumivu makali sio kisingizio cha kuishi kinyume na maagizo ya neno la Bwana. Unaweza pia ukajifunza hilo kupitia maisha ya Ayubu ambaye alipata majaribu makali sana lakini akakataa kumtukana Mungu, kwa sababu ya matatizo aliyokua nayo. Hata hivyo kumuasi Mungu hakupunguzi matatizo, bali kunafanya matatizo na maumivu yaongezeke.

## 02: Kipimo cha Imani kwa Danieli na Rafiki Zake.

- **Kwanza**: Wanapewa elimu ya Kikaldayo na wanaahidiwa vyeo, kwamba walikua katika maandalizi ya kutengenezwa ili wafae kusimama mbele ya mfalme (f. 5)

- **Pili**: Wanabadilishwa Majina Halisi na Wanapewa Majina ya Kipagani (f. 7)
    - Danieli = "Mungu ni Hakimu wangu," Belteshaza = "Bel ndiye mlinzi wa maisha yako."
    - Hanania = "Bwana ni mwenye Neema," na Shadrach = "Mtukuze Aku."
    - Mishael = "Aliye wa Mungu," Meshaki = "Utakua Aku atakavyotaka uwe."
    - Azaria = "Bwana ndiye anisaidiaye," Abed-Nego = "Mtumishi wa Nebo."
- **Tatu**: Wanapewa mtihani wa kula vyakula na kunywa vinywaji ambavyo Mungu amevizuia katika neno lake (f. 8), lakini walisimama imara na walisinda.

## 03: Mungu huwapa thawabu waaminifu hivyo mateso yanaukomo

> Waebrania 11:6 ... kwa maana mtu amwendeaye Mungu lazima aamini kwamba yeye yuko, na kwamba huwapa thawabu wale wamtafutao.
>
> 17 Basi, kwa habari za hao vijana wanne, Mungu aliwapa maarifa na ujuzi katika elimu na hekima; Danieli naye alikuwa na ufahamu katika maono yote, na ndoto.

Baada ya kusimama imara katika majaribu, Mungu alimuita Danieli kuwa nabii na waziri mkuu; huku rafiki zake wakiwekwa kuwa wakuu wa majimbo. Jambo la kujifunza hapa ni kwamba, kila jaribu lina mwisho wake, na unaposimama imara huwa kunakua na thawabu njema ambayo daima Mungu huwapatia wale wanaomchagua.